**Taarifa kwa Wanahabari**

**Afrika inaongoza katika maendeleo ya kukubali mazao ya kibayoteki wakati idadi ya nchi zinazokubali kibayoteki zimeongezeka mara mbili-Taarifa ya ISAAA** :

**Jumatatu, Desemba 7, 2020, NAIROBI** - Afrika imeongeza mara mbili idadi ya nchi zinazopanda mazao kibayoteki kutoka nchi tatu katika mwaka 2018 hadi nchi sita katika mwaka wa 2019, ikiongoza maendeleo kati ya maeneo ya ulimwenguni yaliyokubali kilimo cha Ugeuzi Jeni-GM. Hii ni kutokana na taarifa ya hivi karibuni ya ulimwenguni.

Shirika la Kimataifa la Huduma ya Upataji na Utumizi wa Kilimo cha *Kibayoteki* yaani (ISAAA) iliyotolewa kuhusu Hali ya Kitandawazi ya Mazao ya Kibiashara ya Kibayoteki/ Mazao Ya Ugeuzi Jeni, ya 2019 (Taarifa Fupi ya ISAAA 55). iliyotolewa kwa njia matangazo ya wavuti (webina) leo.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa Ethiopia, Malawi, na Nigeria kuwa ndizo nchi za hivi karibuni zaidi kupanda mazao ya Ugeuzi Jeni (GM) ikijiunga na Afrika Kusini, Sudani, na Eswatini. Nchi hizo sita zinalima mazao matatu ya kibayoteki- mahindi, maharagwe ya soya, na pamba- kwenye takribani hekta milioni tatu kufikia mwishoni mwa 2019. Nchi ya saba, Kenya ilitoa kibali cha kulima Pamba ya Kibayoteki na hivi karibuni itaungana na wanachama wa mataifa ya bara la Afrika waliyoyakubali mazao hayo. Nigeria iliidhinisha upandaji wa kunde ya Kibayoteki yenye maganda ya kuhimili kutobolewa na wadudu (PBR) na kuongezea zao jipya la kibayoteki kwenye mkusanyiko wa kapu la kibayoteki kiutandawazi ; taarifa ilisema.

Vile vile Afrika ilirekodi maendeleo makubwa kwenye utafiti wa mazao ya kibayoteki, kuyarekebisha na kuyakubali kama ilivyoonekana huko Msumbiji, Niger, Ghana, Rwanda na Zambia.Kulingana na ripoti hiyo, Niger imekuwa nchi ya hivi karibuni zaidi kupitisha sheria yao ya usalama.Rwanda ilijiunga na Kenya na Uganda kwenye kufanya utafiti wa muhogo wa Ugeuzi Jeni wakati Zambia iliidhinisha uagizaji wa mazao ya ugeuzi jeni.Msumbiji ilikamilisha uwekaji pamoja wa ombi la kutolewa kwenye mazingira kwa mahindi ya kibayoteki wakati Ghana ilipitisha chombo cha kutunga sheria ambacho kingewezesha ukaguzi wa usalama wa mazao ya kibiashara ya Ugeuzi Jeni.

Wakulima wengi barani Afrika wameonyesha kuongezeka kwa ufahamu na kuithamini bayoteknolojia. Viongozi wa wakulima hasa nchini Kenya, walionyesha matumaini mapya katika kuanza tena kilimo cha pamba chenye faida katika 2020. “ Pamba ya kibayoteki inanipa fursa nzuri sana ya kuitunza familia yangu na baadae kuwapatia watoto wangu maisha salama” alisema

Francis Apailo, mkulima wa pamba wa magharibi ya Kenya kutokana na ufahamu zaidi kuhusiana na teknolojia hii, wakulima wa Kiafrika wanategemewa kukubali mazao ya kibayoteki, ambayo yataathiri familia zao na bara kwa ujumla.

Afrika imechukuliwa kama eneo lenye uwezo mkubwa wa kufaidika kutokana na kupitishwa kwa mazao ya kibayoteki kwa sababu ya changamoto kubwa zinazohusiana na uvamizi mpya wa wadudu na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Kutokana na ongezeko la nchi tatu za Kiafrika, idadi ya nchi zilizopanda mazao ya kibayoteki katika mwaka 2019 zimeongezeka hadi 29 kutoka nchi 26 katika mwaka wa 2018. Nchi tano kuu zenye eneo pana Zaidi za mazao ya kibayoteki zilikuwa Marekani, Brazil, Ajentina, Kanada na India. Kutokana na kiwango kikubwa cha mazao makuu ya kibayoteki kwenye nchi hizi , takribani watu bilioni 1.95 au asilimia 26% ya ulimwengu walipata faida za bayoteknolojia katika mwaka 2019.

Kwa ujumla, hekta milioni 190.4, za mazao ya kibayoteki zilipandwa katika nchi 29 mnamo 2019, na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye usalama wa chakula,uendelevu, kupunguza mabadiliko ya hali ya hewa, na kuinua maisha ya hadi wakulima milioni 17 wa kibayoteki na familia zao ulimwenguni kote.Ukuaji wa kiwango kwa tarakimu mbili katika eneo la kilimo cha kibayoteki kilirekodiwa katika nchi zinazoendelea, hasa Vietnam, Ufilipino na Kolombia.

“Kuiweka Afrika kuwa kiongozi badala ya kuwa mfuasi tu wa kuikubali teknolojia kunahitaji nia njema ya kisiasa katika kiwango cha Umoja wa Afrika, kutumia ubunifu wa wataalamu wake wachanga kupitia kwenye ukuaji wa ujasiria mali hai na upeo mpya wa ST & I. Kwa mapinduzi ya 4 ya viwanda kama vile Biolojia ya Viumbe. Muhimu, kushikilia miungano ya kikanda kwa wale walio tayari itaharakisha ukuaji huu kwa kuboresha ushiriki wa data, utaalamu na ushirikiano kwenye bara lote” alisema Dkt. Margaret Karembu, Mkurugenzi wa ISAAA AfriCenter.

Kwa habari zaidi, juu ya ripoti wasiliana na:
Dkt. Margaret Karembu.
Mkurugenzi , ISAA AfriCenter
S.L.P 70 (00605) ,Uthiru,
Nairobi Kenya.
Simu: +254204223618
Simu ya mkononi: +254722826154
Barua pepe: mkarembu@isaa.org

ISAAA ni Shirika lisilo la faida la Kimataifa ambalo linashiriki kwenye faida za kilimo cha bayoteknolojia ya mimea kwa washika dau mbalimbali, hasa wakulima wenye changamoto za kupata raslimali katika nchi zinazoendelea, kupitia mipango ya kugawana maarifa na msaada wa kueneza matumizi ya wamiliki wa bayoteknolojia. Kupitia mtandao wa ISAA wa kugawana maarifa ulimwenguni na ushirikiano katika mwendelezo wa utafiti na maendeleo, habari yenye msingi wa kisayansi zinauwezesha umma kutoa uamuzi sahihi juu ya kukubali bayoteknolojia na kuitumia.